**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

# UFAFANUZI KUHUSU KIBANDIKO KILICHOWEKWA KWENYE MIFUKO YA SULPHUR YA UNGA CHAPA BENS SULPHUR ILIYOINGIZWA NCHINI MSIMU WA 2023/2024

Bodi ya Korosho Tanzania inapenda kutoa ufafanuzi kuhusu picha mjongeo inayozunguka kwenye mitandao ya kijamii ikionesha mifuko iliyohifadhi sulphur ya unga chapa bens yenye kibandiko inayoonesha maandishi ‘‘GOVERNMENT CASHEW SUBSIDY 2024/2025 CROP SEASON NOT FOR SALE (HAIUZWI)’’ ambapo ukiondoa kibandiko hicho yanaonekana maandishi ‘‘GVT/RUZUKU/2023/2024 NOT FOR SALE’’.

Ukweli ni kwamba maandishi hayo hayana uhusiano wowote na tarehe ya kuisha kwa muda wa matumizi (Expiry date) wa kiuatilifu hicho ambacho kinatumika kuzuia ugonjwa wa ubwiriunga kwenye zao la korosho hapa nchini. Maandishi hayo lengo lake ni kuonesha msimu ambao sulphur hiyo imesambazwa kwenda kwa wakulima. Kibandiko chenye 2024/2025 CROP SEASON kinamaanisha sulphur hiyo imesambazwa msimu wa 2024/2025 ikiwa ni maandalizi ya uzalishaji wa korosho ghafi msimu wa 2025/2026. Kibandiko hicho kimewekwa ili kutofautisha na mifuko ya sulphur chapa ‘bens’ iliyosambazwa msimu wa 2023/2024 kwa ajili ya maandalizi ya uzalishaji wa korosho msimu wa 2024/2025. Kwa mujibu wa maandishi yaliyopo kwenye mifuko hiyo tarehe ya kutengenezwa kwa sulphur hiyo ni Septemba, 2024 na tarehe ya kuisha muda wa matumizi ni Agosti, 2026.

Aidha, lengo la kuagiza sulphur hiyo mapema yaani msimu wa 2023/2024 ilikuwa ni kwa ajili ya kusambazwa katika misimu miwili; msimu wa 2023/2024 na 2024/2025 ili kuhakikisha kwamba wakulima wanapata pembejeo mapema. Ndio maana katika msimu uliopita na msimu huu sulphur ilianza kusambazwa kwa wakulima mapema mwezi Aprili, 2025 tofauti na miaka ya nyuma ambapo usambazaji wa sulphur umekuwa ukichelewa na hivyo kuathiri uzalishaji.

Hivyo kupitia ufafanuzi huu napenda kuwajulisha wakulima wa korosho na umma kwa ujumla kwamba, sulphur hiyo chapa ‘bens’ inayosambazwa sambamba na sulphur chapa zingine haijaisha muda wa matumizi na inafaa kwa ajili ya matumizi ili kukinga ugonjwa wa Ubwiriunga. Aidha, kabla ya kusambaza, sulphur hiyo ilihakikiwa ubora wake na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (Tanzania Plant Healthy and Pesticide Authority – TPHPA).

IMETOLEWA NA:
**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
12 JULAI, 2025